

**SABABU ZA UPOGO WA MALEZI YA MTOTO WA KIUME KATIKA RIWAYA TEULE
ZA ADAM SHAFI**

Subira Makame Mohamed

makameayubmakameali@gmail.com

School of Swahili and Foreign Languages

Department of Swahili

Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA)

Received: April 2024 2024, Accepted June, Published June 2024

© SUMAIT University Journal 2024

Abstract

Authors of literary works discuss several issues of success and problems facing societies. Many of these issues reflect reality of societies. The Swahili literature discusses widely family issues by relating them with forces that contribute to the destruction of family strength. Authors of novels have not ignored the issue of male child care and the challenges that are faced. They see it as a crosscutting issue and have therefore decided to openly discuss it to find solution.

Various literature scholars including Gitau (2005), Kobia (2008), Omari (2008), Jilala (2010/2011), Kobia and Mung'ahu (2013), Khatibu (2014), Lyimo (2014), Noordin (2017), Mosha (2018), and Bayyo (2020), have emphasised issues of gender's responsibility and humiliation.

Some authors of novels are among those who discussed the male child care indicating the way the children are brought up in the society. They have seen that despite some parents efforts to take care of the children, they are still far away from grasping parents teachings (Mbogo, 2005).

The purpose of this paper is to discuss the issue of abusing boys as indicated in the Adam Shaf's novel. During the discussion we shall explain factors that contribute to the phenomenon to a large extent.

Ikisiri

Waandishi wa kazi za kifasihi wanayajadili masuala mbalimbali ya kijamii yakiwemo mafanikio na matatizo. Mengi ya mambo hayo yanawakilisha matendo halisi ndani ya jamii. Fasihi ya Kiswahili inajadili kwa upana matendo ndani ya familia kwa kuhusisha na nguvu zinazochangia kuharibu uimara wa familia. Waandishi wa riwaya hawakufumba macho yao kuhusu suala la malezi ya mtoto wa kiume na masaibu yanayomkabili. Wanaona kuwa hili ni suala mtambuka.

Hivyo, wameamua kulifichua na kuliweka hadharani ili wanajamii walione na waweze kulitafutia ufumbuzi wake.

Wataalamu mbalimbali wa Fasihi, wakiwamo Gitau (2005), Kobia (2008), Omari (2008), Jilala (2010/2011), Kobia na Mung'ahu (2013), Khatibu (2014), Lyimo (2014), Noordin (2017), Mosha (2018), na Bayyo (2020) wametilia mkazo masuala ya jinsia kwa kuonesha kuwa kuna mgawanyo wa majukumu ya kijinsia, pamoja na masuala ya unyanyasaji. Aidha, waandishi wa riwaya ni mionganini mwa wanafasihi waliolijadili na kulishughulikia suala hili la malezi ya mtoto wa kiume kwa kuonesha namna mtoto huyo anavyolelewa katika jamii. Wameona kuwa licha ya baadhi ya wazazi kujitahidi katika malezi ya watoto wao, bado kuna tatizo la kuwekwa mbali na mafunzo ya wazazi (Mbogo, 2005). Makala haya yamekusudia kujadili sababu za upogo wa malezi ya mtoto wa

kiume katika riwaya teule za Adam Shafi. Katika juhudii za kutafuta sababu, tutaeleza namna mambo mbalimbali yanayochangia kuharibika kwa tabia za mtoto wa kiume kwa kiasi kikubwa.

Keywords: Sababu Za Upogo, Mtoto, Riwaya Teule

1.0 Utangulizi

Suala la malezi ya watoto katika taaluma ya jamii limekuwa likijitokeza sana kutokana na umuhimu wake. Wakati mwingine malezi ya watoto hubainishwa waziwazi na waandishi wa kazi za kifasihi kama ni mbinu muafaka ya kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Kwa mfano, Othman (2018) anaeleza kwamba suala la malezi ya watoto ni changamoto kwa wazazi na jamii kwa jumla. Hivyo, jamii inapaswa kujitambua na kuchukua tahadhari. Pamoja na mmong'onyoko wa maadili katika malezi ya watoto kujadiliwa kwa upana wake na wataalamu mbalimbali na kuchukuliwa kuwa ni kawaida, bado sababu za upogo wa malezi ya mtoto wa kiume hazijabainishwa kwa uwazi katika riwaya teule za Adam Shafi. Kwa mantiki hiyo, kuna haja ya kuchunguza sababu zake ili kupanua uelewa katika uga wa fasihi na kwa wanajamii kwa ujumla. Makala hii ina lengo la kuzonesha sababu hizo za upogo wa malezi ya mtoto wa kiume katika riwaya teule za Adam Shafi. Aidha, ni vyema pia kueleza ni mtoto yupi hasa tunayemzungumzia katika makala haya. Katika jamii dhana ya mtoto inaweza kufasiriwa kwa mitazamo tofauti. Kwa mujibu wa makala haya fasili ya neno 'mtoto' linamaanisha kuanzia mtu wa umri wa miaka 8 -17 ambaye kimalezi yupo chini ya uangalizi wa wazazi ama walezi wake, ambaye jamii haijampa mamlaka kamili ya kujitawala hasahaha katika kujiamulia mambo yake.

2.0 Kiunzi cha Nadharia

Makala haya yameongozwa na mwega wa kinadharia wa Shosholojia. Sosholojia ya Fasihi ni kitengo maalumu cha uchunguzi ambacho humulika mahusiano baina ya kazi ya sanaa, namna ya muundo wa kijamii, na jinsi kazi hiyo ilivyojitokeza na kutathminiwa ubora na udhaifu wake. Nadharia ya Sosholojia inamhusisha mzazi kuwa ni nguzo kuu katika ujenzi wa familia bora, yaani inaonesha uhusiano wa mzazi na mtoto. Katika makala hii, msingi uliotumika ni ule unaoleaza kuwa mzazi ni nguzo kuu katika ujenzi wa familia bora (uhusiano wa mzazi na mtoto). Jamii zote zimeendelea kuitia dini, metafizikia, na sayansi. Jamii zinahitaji elimu ya kisayansi yenyе misingi ya ukweli na ushahidi kutatua matatizo yake, na siyo uvumi na ushirikina (Comte, 1839) ambaye alikuwa ni mwanasosholojia. Hali ya majukumu ya wazazi na walezi kuwa ndio nguzo kuu katika ujenzi wa familia bora ndiyo pia hujitokeza katika riwaya teule za mwandishi teule ambazo zina mwelekeo wa kimalezi.

Methodolojia ya utafiti

Data ya makala hii imepatikana kutoka katika sampuli ya vitabu vitatu teule vya Adam Shafi. Kwa kuvitaja, ni riwaya za Kasri ya Mwinyi Fuad (2008) Mbali na Nyumbani (2013), na Mtoto wa Mama (2018). Uteuzi wa vitabu hivyo vitatu kama Sampuli umefanyika kwa mbinu ya usampulishaji lengwa. Hii ni kwa sababu humruhusu mtafiti kuwachagua wawakilishi wa kutafitiwa kulingana na jinsi wanavyokidhi haja na malengo ya utafiti wake. Aidha, baadhi ya data za makala haya zimepatikana kuitia mbinu ya usaili na majadiliano ya vikundi lengwa. kutoka kwa wanafunzi thelathini wa Shahada ya Kwanza wanaosoma masomo ya Fasihi ya Kiswahili kutoka katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Dr. Abdulrahman Al

Sumait, na Chuo Kikuu cha Zanzibar (Z.U). Kwa ujumla, makala imeteua vitabu hivyo kwa kuzingatia kuwa suala la malezi ya mtoto wa kiume limejitokeza katika riwaya tajwa.

Matokeo ya utafiti

Kudekezwa

Kwa mujibu wa Santrock (2007), walezi wanaodekeza watoto, hutokana na kuwapenda watoto wao kupita kiasi. Hawatungi sheria zozote za kuwaongoza watoto wao. Huwaacha huru wafanye watakalo. Kulingana na Ngwiri (2008), kuna tofauti kati ya wazazi wanaodekeza na wanaopendelea. Anaeleza kuwa, wazazi wanaodekeza watoto hawaweki sheria zozote za kuwaongoza watoto wao. Watoto hufanya wapendalo. Kupitia riwaya ya *Kasri ya Mwinyi Fuad* mwandishi ameionesha hali hiyo kwa Bwana Malik na Bibi Maimuna namna wanavyomdekeza mtoto wao wa kiume kwa kuwa ni mtoto pekee na mrithi wa familia hiyo. Kulithibitisha hili mwandishi anasema:

Fuad alikuwa ni mtoto mkubwa mwenye umri wa kiasi cha miaka mitano na mtundu wa kutosha... Kutwa alikuwa anavunja vitu ndani ya nyumba na alipenda mchezo wa kuchupa huku na huku. Alikuwa anaweza kufanya jambo lolote au kusema kitu chochote mbele ya mtu yeyote na kwa yote haya hakuna aliyeweza kumkanya kwa kuchelea kutukanwa ama na Bwana Malik au na Bibi Maimuna. Alidekeza kupita kiasi na kila alilolifanya yeye lilikuwa sawa kwa wazee wake. (uk. 2)

Dondoo hili linaonesha namna malezi ya wazazi hao walivyochangia kupotoka kwa mtoto huyu wa kiume ambaye alitarajiwa kuwa mrithi wa familia.

Kupitia riwaya ya *Mtoto wa Mama* mwandishi ameionesha hali hiyo kwa Zamda anavyompenda kupita kiasi kama ni mtoto pekee wa kiume ambaye amekosa penzi la baba yake baada ya kufungwa jela tangia yungali mtoto mchanga. Licha ya unyonge wake Zamda alimlea kwa mapenzi mazito mtoto huyo. Kulithibitisha hili mwandishi anasema:

Zamda aliichukua kanga aliyokuwa amejitanda akajifuta machozi, akamfuta na Saburi machozi yaliyokuwa yamemjaa tele usoni, yanatiririka njia mbilimbili (uk.42).

Hapa tunaona jinsi mtoto huyu wa kiume anavyodekezwa kwa kujiegemeza katika ubavu wa mama yake.

Kwa upande wa riwaya ya *Mbali na Nyumbani* hali hii imedhihirishwa na mwandishi kupitia Ahmada alivyopendwa kupita kiasi na baba yake. Ahmada alizawadiwa na baba yake kitambaa cha thamani alichopewa na rafiki yake kutoka Ngazija ili avae siku ya harusi yake. Hakufanya hivyo, kutokana na mapenzi makubwa aliyokuwa nayo alimzawadia mwanawе mpenzi. Kwa nafsi yake anaeleza kwamba hakuja kuwa alikuwa akipendwa na baba yake mapenzi ya kupitiliza, Ahmada anasema:

*...Nilipomtazama niliyahisi mapenzi yake
ya dhati aliyokuwa nayo kwangu. "Mimi
sina cha kukupa mwanangu," alinambia. Nilimtazama
tena. Nilimwonea huruma kwani nilikuwa na hakika*

*kwamba chochote ambacho ningelikitaka wakati ule
basi angelinipa kama angelikuwa nacho (uk. 436 - 437).*

Dondoo hili pia linaonesha jinsi baba yake Ahmada alivyoathirika kwa kumpenda mwanawe mapenzi ya kupitiliza. Kulingana na nadharia ya sosholojia, kupitia msingi wake unaoeleza kuwa mzazi ni nguzo kuu katika ujenzi wa familia bora, unaoangalia (uhusiano wa mzazi na mtoto), tunaona kwamba umetuwezesha kuelewa sababu za upogo wa malezi ya mtoto wa kiume katika riwaya teule za Adam Shafi juu ya suala hili la kumlea mtoto kwa kumdekeza na kumpenda mapenzi ya kupitiliza. Imebinika kuwa wazazi ni sababu moja wapo ya upogo wa malezi ya mtoto wa kiume kupitia riwaya teule za mwandishi.

Umagharibi

Kufuata umagharibi ni kitendo cha kufuata mila, hulka, silka, mienendo na tamaduni za kigeni. Moja katika sababu ambazo zinayafanya malezi ya watoto wa kiume kwenda kinyume na matarajio ya jamii ni kufuata utamaduni wa kigeni. Kwa mujibu wa Madumulla (1995), waandishi wa riwaya ya Kiswahili wanaonekana kuandika riwaya zenye kubeba mwigo wa nchi za kimagharibi ambazo huwa kama sinema zinazoonesa matukio ya kigeni kwa kutumia wahusika, lugha, na mandhari ya Kitanzania.Utandawazi umefungua mipaka ya watu na kuingiza tamaduni za kigeni katika nchi nyingine kama za Afrika. Jambo hili linazifanya nchi za kimagharibi zenye nguvu kiuchumi na kiteknolojia, kusambaza utamaduni wao kwenda katika nchi nyingine hasa za Afrika. Hali hii ndiyo inayojitokeza kupitia riwaya ya *Mtoto wa Mama*. Saburi anachelewa kurudi nyumbani kwao kwa sababu ya kumsindikiza msichana. Saburi anamsindikiza Mwajabu wakati anarejea nyumbani kwao. Zamda anahoji:

“Mbona umekawia ?”.... Nilimsindikiza Mwajabu kwao,”

alijibu Saburi. . “...

“En!” Alishangaa Saburi.

Chechele anaweza akawa hata mtu, kama huyo

Mwajabu aliyekupoteza njia ukamfikisha

mpaka kwao, (uk. 133).

Kwa upande wa riwaya ya *Mbali na Nyumbani* mawazo kama haya yanajitokeza tena kwa watoto hao wa kiume mwishoni mwa wiki, huelekea mjini kuangalia sinema. Imebainika kwamba, watoto wa kiume huangalia sinema na kupitia sinema hujifunza mambo mbalimbali yanayokiuka utamaduni wa Kizanzibari. Ahmada anaeleza:

*Jumamosi, wakati wanafunzi wenzangu wakienda
kutembea majumbani kwao kuwatemeblea wazazi
wao au wakienda mjini kwa matembezi ya kawaida
na kujiburudisha kwa kuangalia sinema, mimi nilikuwa,kazini (uk. 9).*

Hapo tunaona namna ambavyo wanafunzi wanavyojoingiza kwa kasi katika kufuata mila za Kimagharibi kwa kuangalia mambo tofauti kila ifikapo mwisho wa wiki kwani hujimwaga kwa wingi mjini kuangalia sinema.

Mwingiliano wa Tamaduni

Kwa namna fulani mwingiliano wa tamaduni huchangia kwa kiasi kikubwa kuharibika kwa malezi ya mtoto wa kiume. Kuhama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine huwafanya watoto wa

kiume kuacha utamaduni wa kwao na kufuata silka na mienendo ya eneo alilo bila kujali litakalotokea.

Hali hii imejitokeza tena kupidia Ahmada wakati akiwa Ujerumani anajinasibu aliquwa akitinga shati ambalo ameshonewa na baba yake akiwa na mabinti wa Kijerumani. Ahmada anaeleza:

*Kama alivyotaka baba yangu, kitambaa alichonipa nilikipeleka
kwa mshonaji na alinishonea suti nzuri. Suti hiyo ilikuwa ndiyo
vazi langu rasmi la kutokea mwisho wa wiki nilipokuwa nikienda
kujirusharusha na kujimwagamwaga na vitoto vyta kijerumani
katika kumbi za starehe za Berlin. (uk. 481)*

Dondoo hili linaonesha namna malezi ya mtoto Ahmada yalivyokwenda kinyume na matarajio ya jamii. Licha ya safari ya kimasomo ambayoaliadhima, alijiingiza katika mambo mengine ambayo ni kinyume na utamaduni wake. Wanachofahamu wazazi ni kwamba mtoto wao yuko masomoni nje ya nchi lakini mtoto mwenyewe tayari ameshajiingiza katika umagharibi.

Kulingana na nadharia ya sosholojia, kupidia msingi wake unaoeleza kuwa mzazi ni nguzo kuu katika ujenzi wa familia bora, unaoangalia (uhusiano wa mzazi na mtoto), tunaona kwamba umetuwezesha kuelewa sababu za upogo wa malezi ya mtoto wa kiume katika riwaya teule za Adam Shafi juu ya suala hili la malezi ya mtoto kwa kufuata umagharibi. Imebinika kuwa umagharibi ni mionganini mwa sababu za upogo wa malezi ya mtoto wa kiume kupidia riwaya teule za mwandishi.

Starehe na Anasa za Kupitiliza

Starehe ni jambo linalompatia mtu raha (BAKIZA, 2010). Mtunzi wa riwaya teule amelionesha hili kupidia kurasa mbalimbali za riwaya hizo.

Ni matarajio ya wazazi wanapowalea watoto wao wakulie katika maadili mema. Lakini watoto wa kiume wanapoingia katika starehe husababisha upogo katika malezi yao.

Kwa upande wa riwaya ya *Mbali na Nyumbani*, tunaona watoto wa kiume wanavyosifiana habari zao. Wanastarehe na wanawake katika mikahawa ya thamani. Mwandishi anaeleza:

*Walikumbuka starehe zao katika mikahawa ya
fahari na wanawake wazuriwazuri. (uk. 35).*

Hapa tunaona watoto hawa wa kiume walivyokuwa wakisifiana upogo wao uliosababishwa na starehe. Wanavyosifiana namna walivyokuwa wakistarehe na wanawake wakiwa katika shughuli zao za kibaharia.

Kwa upande wa *Kasri ya Mwinyi Fuad* mwandishi amelijadili suala la starehe katika kurasa mbalimbali za kitabu hicho kama ifuatavyo:

*Alistarehe kama kijana yeyote yule mwenye
pesa nyingi (uk. 24).*

Kwa maelezo hayo tunaona kuwa suala la starehe lilisababisha upogo wa malezi ya mtoto wa kiume kwa asilimia kubwa. Aidha, mwandishi anafafanua tena starehe zilivyokuwa ndio msingi mkuu wa upogo wa malezi ya mtoto wa kiume wa jamii ya Wazanzibari.

Kwa upande wa riwaya ya *Mbali na Nyumbani* mwandishi ametubainishia sababu za upogo wa malezi ya motto wa kiume kupitia starehe zinazofanywa na watoto hao, ambao walijimwaga katika maeneo ya baa na kumbi mbalimbali za starehe kwa lengo la kutabaradi. Mwandishi ametubainishia hilo kupitia Ahmad, Suleiman na wenzao ambao walijimwaga katika maeneo ya baa na kumbi mbalimbali za starehe kwa lengo la kutabaradi. Ahmad anaeleza:

“Twendeni tukatabaradi kidogo,” alitushauri... “Wapi?” “Hapo juu ,” alituonyesha kule kwenye ghorofa ya kwanza ya hoteli ile. “Tutatabaradi vipi na pesa hatuna, Hussein alimwuliza tena. “Mimi nnazo dola ishirini,” alisema. “Twenty Dollars!” alitilia mkazo kwa Kiingereza. “Twendeni,” alisema. (uk. 456 - 457).

Mwandishi analalamikia watoto wa kiume kuhusu masuala haya kwa sababu wimbi kubwa la watoto tayari wameshatumbukia katika dimbwi la starehe ambalo kwa kiasi kikubwa linachangia katika kuendeleza upogo wa malezi ya mtoto wa kiume wa jamii ya Wazanzibari.

Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* mwandishi amemwonesha Shauri namna alivyotamba kwa masuala ya starehe. Alistarehe nyumbani kwake na wanawake katika maeneo ya fukwe mbalimbali kwa unywaji wa vimeo na muziki.

Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa, watoto wengi wa kiume hujihusisha na masuala ya starehe kutokana na kukosa mahusiano mazuri baina ya watoto na wazazi wao. Hatimaye watoto hao kila uchao hubadilisha mazingira mapya ambayo yatawapa faragha zaidi ili kuendelea na upogo huo. Mwandishi anaeleza:

*Alipochoshwa na starehe za pale kwake, Shauri alianda
mandari mahali pengine ili kubadili mandhari. Siyo
ufukweni tena kwani mandhari ya ufukwe ndiyo
hayo yaliyokuwa yamemchosha... (uk. 3 - 4).*

Hapa tunaona jinsi mwandishi alivyoibainisha kuwa starehe ni chanzo cha kumong’onyoka kwamaadili ya watoto. Kulingana na nadharia ya sosholojia, kupitia msingi wake unaobainisha uhusiano wa mzazi na mtoto, umetuwezesha kuelewa sababu za upogo wa malezi ya mtoto wa kiume katika riwaya teule za Adam Shafi juu ya suala zima la kupenda mno starehe na anasa, inaonekana kuwa ni kikwzo cha maendeleo katika malezi ya watoto wa kiume. Wengi wao wamepotoka kutokana na suala hili.

Ajira za Watoto

Kavuria (2008) akizungumzia unyonywaji wa watoto, anaeleza kuwa, watoto hunyanyaswa kwa kuajiriwa kama wasaidizi wa kazi za nyumbani au kufanyishwa kazi nyingi zilizopita umri wao. Watoto wa kiume katika riwaya teule wanaonekana kama ni kundi moja wapo linalojihusisha na ajira za watoto. Watoto hao hujiingiza katika ajira hizo kwa sababu ya kujipatia huduma zao na wakati mwingine mahitaji ya familia zao aidha, kwa kutelekezwa au kusambaratika kwa familia. Hii inawezekana kwa kufariki mmoja kati ya wazee wa mtoto, talaka au hata masaibu yanayowakumba walimwengu kama kutekwa na kufungwa jela (gerezani).

Kupitia riwaya teule za Adam Shafi suala hili kalijadili kwa upana wake. Kwa kuanza na riwaya ya *Mtoto wa Mama* suala la ajira kwa watoto limejadiliwa na mwandishi. Kutokana na umasikini aliokuwa nao mama wa mtoto huyo, alimshirikisha mtoto wake katika biashara yake ya mikate ili waweze kujikimu kimaisha. Mwandishi anathibitisha:

*Saburi alikuwa katikati ya vurumai iliyokuwepo Njia Kuu.
Sauti ya kitoto ilisikika kwa mbali ikiinadi mikate yake.”
Haya mikate motomoto!*

Haya mikate motomoto (uk. 55)

Kitendo cha Saburi kutokwenda shule kilimfanya kutumbukia katika dimbwi la ajira ya kuuza mikate ambayo ilitengenezwa na mama yake, aliuza mikate hiyo mitaani na hata Mbele ya Njia Kuu. Baadhi ya wazazi hawapendi hata kidogo watoto wao kujishughulisha na kuuza biashara ila sababu ya umasikini na hali ngumu ya uchumi iliyotawala katika kaya zao huwalazimkia kuwashirikisha watoto wao wa kiume katika ajira zao bila kujali athari zinazoweza kutokea. Hapa tumeona jinsi Saburi alivyokuwa na ajira ya kuuza mikate kwa lengo la kujipatia mahitaji yake.

Hapo tunaona jinsi mtoto wa kiume Saburi, alivyojishirikisha katika ajira mbalimbali za utotoni kama vile biashara ya kuuza mikate. Mtoto huyu alijituma ili kupata mahitaji yake pamoja na mahitaji ya mama yake. Hapo tunaona jinsi mtoto wa kiume alivyokwenda kinyume na matarajio ya jamii. Ni matarajio ya jamii, mtoto wa kiume kama Saburi asome kwanza na muda wa masomo ukimalizika abaki nyumbani akimsaidia mzazi wake kazi ndogondogo anazoziveza. Baada ya hapo basi awe anashirikiana na wenzake katika michezo yao ya kitoto. Kutokana na Saburi kukosa nafasi ya kwenda shule kulimsababishia kuijingiza katika ajira tofauti ikiwemo ya kuuza mikate. Huu ni upogo ambaulisababishwa na ajira za utotoni, ajira ya kutembeza sinia ya mikate.

Kulingana na nadharia ya sosholojia, kupitia msingi wake unaoeleza kuwa mzazi ni nguzo kuu katika ujenzi wa familia bora, umetuwezesha kubaini sababu za upogo wa malezi ya mtoto wa kiume katika suala la kuajiriwa watoto. Inaonekana kuwa uhusiano bora kati ya mzazi na mtoto wake kutokana na mtoto huyo kushindwa kupata stahiki zake za msingi kutoka kwa mama yake na kuangukia katika biashara za mikate na uchukuzi wa mizigo. Kutokana na ajira, watoto hupata nafasi ya kutenda mambo tafauti yasiyoridhiwa na jamii.

Vikundi Viovu

Makundi ni mkusanyiko wa watu au vitu ambavyo vinaonesha ukaribu wa pamoja au mkusanyiko wa pamoja. Marafiki ni watu ambaulisababishwa wanakuzuwa ni maswahibu wa watu. Watoto hao huwa na mtandao mpana wa marafiki, na swahiba zao. Marafiki huaminika na kupewa siri zote na kwa vile huaminiana mara nyingi siri hizo si rahisi kuvuja. Ushawishi rika hutoa mchango mkubwa katika kuwafanya watoto wa kiume waende upogo. Ushawishi huo unaotokana na makundi ama vikundi vyta marafiki wabaya huwachanganya watoto hao na kusababishwa kubadili mielekeo yao.

Watoto wa kiume wanapokuwa pamoja na rafiki zao huunda makundi na vigenge ambavyo kwa namna moja ama nyingine huathiriana kutokana na kushawishiana kwao na hata kuambukizana tabia mbaya. Baadhi ya wakati watoto huchagua marafiki wasiofaa na kuambukiza tabia mbaya. Tabia hizo kwa vile wako pamoja muda wote hurithishana. Tabia zenyewe ni kama vile ulevi, uzinzi, wizi, ulawiti, ukabaji na hata ujambazi.

Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, mwandishi amejadili namna marafiki na vikundi vinavyochangia kwa watoto wa kiume kwenda upogo. Mwandishi amemwonesha Saburi kuwa ni mtoto wa kiume ambaye hufuata marafiki kwenda kule ambako mama yake hakufahamu na hajui malengo ya safari ya mtoto wake huyo. Kitendo cha Saburi kufuata marafiki kulimtia wasiwasi na wahaka mama yake. Imebainika kuwa watoto wa kiume wanapokaa katika makundi na marafiki zao mbalimbali

hushawishiana kutenda mambo ambayo hayaridhiwi na wanajamii. Hali hii inathibitishwa na mwandishi katika uk.55:

Mawazo yake yote yalikuwa kwa Saburi. Hakujua alikokwenda, hakujua amefikwa na masaiibu gani, hakujua alikutana na ibilisi gani aliyezemzaini akamtia ushetani wa kwenda huko alikokwenda. Hakutaka kurudi nyumbani kwani wakati ule ilikuwa ni mapema mno kufanya hivyo. Aliikiuka Njia Kuu akaingia vichochoroni na ghafla alitokezea kwenye uwanja mkubwa uliokuwa umejaa watoto... (uk. 55)

Hapa tunaona Zamda anavyopata shida kutokana na malezi ya Saburi ambapo Saburi mwenyewe hajali kuhusiana na hili.

Kwa upande wa riwaya ya *Mbali na Nyumbani* mwandishi amelielezea suala hili. Mwandishi anamsawiri Ahmada alivyokuwa akizurura kutafuta wenza wa mashauri akiwa katika lengo la kufanikisha safari yake ya kuwenda masomoni nchi za Ulaya. Kwa mfano, Ahmada anasimulia:

Hapo ndipo nilipowakuta wazururaji wenzangu wasiokuwa na kazi kama mimi. Nilikaa nao nikisikiliza hadithi zao za kibaharia (uk. 35)

Tunaona Ahmada akitafuta kundi la mabaharia alipofika Mombasa, kama ni sehemu ya kujipoza machofu ya safari kwa masahibu wake kutoka Zanzibar, waliokuwa wakifanya kazi ya ubaharia katika mji wa Mombasa. Hali hii inadhihirisha mwenendo mahsusini wa kundi rika hili.

Baadhi ya watoto wa kiume walijilingiza katika makundi na mwishowe kushiriki katika vitendo viovu. Baadhi ya wakati watoto hao huweza kufuata makundi kimkumbo, hawana mchango wowote juu ya kundi hilo. Wanaweza kufuata kundi jema au kundi ovu. Hali hii mara nyingi anayefuata hivyo anakuwa dhaifu. Anategemea msaada kutoka kwa wengine. Vile vile, Ahmada anaeleza kwa kusema:

...Kwakuwa mimi nilichukuliwa tu, sikuwa na hata senti moja mfukoni mwangu na maisha yangu yote wakati wa safari yetu hiyo yalitegemea takrima ya wenzangu wawili wale, basi mimi nilikuwa nikifuata tu. Kwangu mimi, lolote waliloliamua wao lilikuwa ni sawasawa tu (uk. 48).

Ahmada anaonekana kufuata mkumbo kwa marafiki zake kutokana na kuwa hakuwa na uwezo wowote wa kujikimu hadi kumfikisha safari yake. Kundi kubwa la watoto wa kiume hujihuisha na makundi na marafiki bila kujiangalia je kundi hilo wanalingana kihadhi na bila kuelewa malengo ya kundi hilo. Mwishowe hujikuta kuwa ni asi kuanzia ngazi ya familia, jamii na hata taifa kwa ujumla.

Hapo tunaona kuwa, vikundi na marafiki wana mchango mkubwa kwa watoto wa kiume kwenda kinyume na matarajio, kutokana na kuwa wanapokaa pamoja huathiriana kitabia. Hivyo, huambukizana tabia mbaya mmoja baada ya mwingine kutokana na kuigana kwao.

Kwa mujibu wa nadharia ya sosholojia, kuititia msingi wake unaoeleza kuwa mzazi ni nguzo kuu katika ujenzi wa familia bora, umetuwezesha kubaini sababu za upogo wa malezi ya mtoto wa kiume kuititia riwaya teule za Adam Shafi juu ya suala la malezi ya mtoto kwa kufuata vikundi viovu. Kujiunga na vikundi viovu ni sababu tosha ya kupelekea upogo wa malezi ya mtoto wa kiume.

Ongezeko la Watoto wa Mitaani

Watoto wa mitaani ni watoto wanaorandaranda kwenye barabara za mji au mitaa wakitafuta vyakula na usaidizi wowote kutoka kwa wakazi wa maeneo hayo. Miongoni mwa sababu kuu za kupatikana kwa watoto hawa ni kuvunjika kwa ndoa na familia masikini ambazo hushindwa kutimiza mahitaji ya msingi ya watoto. Watoto wa mitaani wanaishi maisha ya kuhamahama na ya muda mfupi. Watoto hawa hawakai mahali pamoja kwa muda mrefu. Utafiti umebaini kuwa moja ya sababu zinazosababisha upogo katika malezi ya mtoto wa kiume ni kuongezeka kwa watoto wa mitaani. Hali hii kama ilivyokwishaelezwa hapo juu kwamba sababu yake kuu ni familia masikini zinazoshindwa kumudu mahitaji muhimu ya watoto pia husababishwa na familia ya upande mmoja.

Katika riwaya teule ya *Mtoto wa Mama* tukio hili limejadiliwa kwa kina na mwandishi. Saburi alikuwa na tabia ya kuzurura katika mitaa na kuelekea asikokujua akitarajia kuwa atarudi na riziki ama usaidizi wowote akiwa katika ziara zake. Tukio lenyewe ni hili:

“Una njaa?” Alimwuliza. Saburi aliitikia kwa kutikisa kichwa tu
huku akifuta machozi kwa shati lake la kaki “Ngoja,”
Bwana Hababuu alimwambia, akaingia ndani. Baada ya muda mfupi,
alitoka ndani mle mwanamke wa makamu aliyejitanda kanga
chafu akiwa miguu chini. Alikuwa na kifurushi kilichokuwa
kimezungwazongwa ndani ya karatasi. Alimpa Saburi kile kifurushi
akamwambia, “Haya nenda zako nyumbani.” “Nyumbani sikujui,”
Saburi alimwambia (uk. 90).

Dondoo hili linaonesha namna malezi ya mtoto Saburi yalivyokwenda upogo. Licha ya Zamda, mama mzazi wa Saburi kujitahidi katika kumuongoza mtoto wake na kumfundisha maadili mema, baadhi ya wakati ilionekana mama huyu kushindwa na mtoto wake. Aliondoka na kuelekea popote anakotaka kwenda hata kama hakuju, na wakati mwinge bila ya mama yake kuelewa. Hii ilitokana na mzazi wa mtoto huyu kushindwa kutimiza mahitaji ya mtoto wake. Hali hii ilimpelekea Saburi kuzurura katika mitaa akitarajia atapata chochote.

Hali hii inaonekana wazi kuwa Zamda alishindwa kumdhibiti mtoto wake kwa kumzuia asiende popote kuzurura. Kwa sababu Saburi alikwishazowe mtindo huu mbaya wa kuzurura katika mitaa na alitoka bila ya hata mama yake kuju ameelekea wapi. Mwisho wa siku Zamda alikatisha kumfuatilia mtoto wake juu ya hilo.

Dondoo hili linaonesha namna Saburi ghafla, alivyokuwa mtoto wa mitaani akipita mitaani na kurudi na vifurushi vya vyakula. Kwa vile Saburi hakuwa na kazi ya kufanya mwishowe, Saburi alihamia Mbele ya Njia Kuu akashirikiana na walevi, majambazi, wizi na wavuta bangi.

5.2.3.8 Hali Ngumu ya Uchumi

Uwezo wa kiuchumi wa wazazi huathiri mbinu watakazotumia kuwalea watoto wao (Francesc, 2018). Anadai kuwa wazazi wenyе kipato cha juu hutumia mbinu tofauti ya malezi ikilinganishwa na wazazi maskini. Anaendelea kusema wazazi wenyе uwezo wa kiuchumi huwadekeza watoto na huwapa elimu bora ambapo watoto ambao wazazi wao ni masikini, hukosa elimu au hupata elimu duni. Pia, wazazi maskini hawana muda wa kukaa na kuwaongoza watoto. Muda wao mwingi huutumia kuwatafutia watoto mahitaji yao ya msingi.

Suala la umasikini katika riwaya teule limesababisha malezi ya watoto wa kiume kwenda kinyume na matarajio ya wanajamii.

Kwa namna nyingine suala la umaskini hujitokeza pale ambapo watoto wa kiume wanapojihusisha na vitendo visivyokubalika katika jamii. Miongoni mwa wanajamii na serikali kwa ujumla hupoteza imani kwa watoto hao hivyo, wanaweza kukoseshwa fursa za ajira. Kutokana na hali hiyo, umaskini huzidi kushamiri katika jamii kutokana na watoto hao kukosa ajira. Hii ni kwa sababu hukosa nyenzo ya kupatia mahitaji yao.

Aidha, upogo wa malezi ya mtoto wa kiume husababisha umaskini kuanzia ngazi ya taifa na familia kwa ujumla. Watoto hao tayari wameshapoteza muelekeo kutokana na kujingiza katika wizi. Mtoto huyu wa kiume hufikia kikomo cha kuiba nyumbani kwao na wakati mwingine huwaibia hata wazazi wake. Kutokana na hali hii, umaskini huzidi kuongezeka katika jamii.

Katika riwaya teule ya *Mtoto wa Mama*, mama mzazi wa Saburi, Zamda anaonekana kuwa kutokana na mazingira magumu aliyokuwa nayo yalimsababishia mtoto wake kwenda upogo. Umasikini wake umechangia kwa kiasi kikubwa kwa mtoto wake huyo wa kiume, katika kumlea kwake aonekane anakwenda ndivyosivyo. Hii ni kutokana na Zamda kutokidhi mahitaji ya mwanawе ikiwemo chakula na mavazi. Mavazi ya kawaida ya Saburi yalimwendesha resi Zamda kutokana na hali yake ya kiuchumi. Ilimuwia vigumu hata nguo za mwanawе zilifikia kuraruka wakati zinapofuliwa kwa zilivyochocha, alizisugua kwa hadhari ili zisije zikachanika mikononi. Mwandishi anatuambia:

Alilitia maji shati na kulisugua kwa sabuni. Alilifilikichafikicha polepolelisije likararuka tena, akalisuuza na kutoka nalo... (uk. 63).

Saburi alichukuwa mfuko na kalasia na baada ya kupewa pesa alimtzama mama yake na kumwambia, "Taa ya chumbani haina mafuta." "Pesa nilizonazo ndo hizohizo," alisema Zamda (uk. 95).

Dondoo hilo linaonesha namna Zamda alivyochocha na hali ngumu ya maisha. Uchumi wake ulidorora na kusababisha mtoto wake, Saburi kutokumsikiliza kwa baadhi ya mambo aliyokuwa akimwelekeza na kumkataza. Baada ya kuoshwa kwa tahadhari shati la Saburi ili lisijekuraruka kutokana na udhaifu wa shati hilo, Saburi bila ya nguo yoyote alikaa kulisubiria shati hilo likauke. Baada ya shati hilo kufikia wastani wake wa kukauka, Zamda alimuita ili alivae asibaki tumbo nje. Nukuu hii inaonesha waziwazi umasikini aliokuwa nao Zamda. Kutokana na unyonge huo alishindwa kumnumulua mwanawе nguo za kushindia na mwisho wake ikamsababishia Saburi kukosa mengi ikiwemo kukosa kusoma elimu ya lazima na kusababisha kuijunga na majambazi na walevi kufanya nao kazi za kubeba mizigo Mbele ya Njia Kuu. Kutokana na hali ngumu ya maisha na umasikini aliokuwa nao mama mzazi wa Saburi, alimnumulua mwanawе nguo za mitumba ambapo Saburi kutokana na hali yao kuwa dhaifu aliziona nguo hizo kuwa ni mpya, ambapo wenye vyao walimuangalia kwa dharau na kumkebehi. Walimwona ni mmoja wa watoto ambao mama zao ni watumishi wanaowatumikia matajiri wanaoishi Majuuumba ya Mawe.

Kwa upande wa riwaya ya *Mbali na Nyumbani*, utafiti umebaini kuwa baadhi ya watoto wa kiume wakiishi ughaibuni kama mafukara. Hawakuwa na pesa za kujikimu. Wengi wa watoto hao waliondoka kwao bila ya ridhaa za wazazi wao. Kutokana na hali hiyo ya kuondoka nyumbani kwao bila ya ruhusa za wazazi na walezi wao, maisha ya watoto hao yaliwawia vigumu, kwa sababu waliishi kwa kujitegemea ambapo hali hiyo hawakuimudu. Ahmada anaeleza:

Na viyi tungelikuwa wasafi? Watu tulikuwa tukiishi kama mafukara
waliokosa mahali pa kuishi (uk. 299).

Dondoo hizo kwa ujumla wake zinatuonesha hali ya umasikini iliyowagubika watoto hao wa kiume wa Kizanzibari walipokuwa katika mazingira tofauti. Watoto hao kwa sababu ya umasikini uliowazonga wao pamoja na familia zao wanaonekana wakienda ndivyosivyo.

Familia ya Mzazi Mmoja

Familia ya mzazi mmoja nayo pia ni mionganoni mwa sababu kubwa iliosababisha mtoto wa kiume kwenda upogo. Hii inatokana na mzazi mmoja hususan wa kike kukosa udhibiti wa kumlea mtoto sambamba na kumkamilishia mahitaji yake.

Pia, kwa kawaida watoto huwaogopa zaidi wazazi wao wa kiume kulikoni wa kike. Hivyo tunaweza kusema kuwa familia ikitoka mzazi mmoja wapo hususan wa kiume basi familia hiyo huchukuliwa kuwa na udhaifu na mapungufu. Saburi alijihisi hana faraja kwa vile hakumjua baba yake isipokuwa katika hadithi za barazani wakiwa na Kibwe. Tunamwona Saburi ambaye kwa bahati mbaya hakupata kulelewa hata siku moja na mzazi wake wa kiume kutokana na baba yake huyo kufungwa gerezani kwa muda usiojulikana. Hili linajitokeza katika uk. 93. Mwandishi anatuambia:

*Zamda alimpenda Saburi kwa sababu
alikuwa ni mwana pekee aliyejaaliwa. Aliyejaaliwa kuwa
naye akiwa baba, Aliyejaaliwa kuwa naye akiwa mama.
Alimwonea huruma kwa sababu Saburi alikosa raha
zote alizostahili mtoto kama yeye, raha ya kulelewa na
baba na mama, raha ya kucheka na baba na mama,
raha ya kudekezwa na baba na mama. Saburi alibakia
kuwa mtoto wa mama tu (uk. 93.)*

Saburi aliendelea kuteseka kutokana na kuwa hakuwa na baba wa kumuhangai. Alitafuta kazi apate pesa ili ajikimu mahitaji yake pamoja na mama yake. Ili azimudu gherama za maisha ilimlazimu azihangaikie. Mama mzazi wa Saburi roho inamuumma kutokana na mwanawewe anavyoteseka na maisha kwa kujitafutia riziki, lakini kutokana na unyonge uliomtawala hakuweza kumnusuru mtoto wake na hali hiyo isipokuwa alimwacha ajihangaikie pamoja na yeye mwenywewe.

Kwa mantiki ya maelezo haya, mwandishi amekusudia kutuonesha jinsi suala la familia ya upande mmoja inavyosababisha upogo wa malezi ya mtoto wa kiume. Tunamwona mwandishi anavyomwelezea Zamda jinsi alivyopambana kumlea mtoto huyo wa pekee tangu mdogo sana hadi walipotengana baada ya nyumba waliyokuwa wakiishi ilipochukuliwa na wanaojiita kuwa ni warithi wa marehemu Mzee Hamisi ambaye ndiye aliyekuwa mmiliki wa nyumba hiyo. Kulingana na nadharia ya sosholojia, kuitia msingi wake unaoeleza kuwa mzazi ni nguzo kuu katika ujenzi wa familia bora, umetuwezesha kubaini sababu za upogo wa malezi ya mtoto wa kiume katika suala la kulelewa na mzazi mmoja.ili malezi yatengenee, mtoto apate malezi ya ushirikiano baina ya bba na mama vyenginevyo, hutokea upogo wa malezi.

Ukosefu wa Haki ya Msingi ya Elimu

BAKIZA (2010) inafafanua kuwa, elimu ni maarifa anayoyapata mtu baada ya kujifunza jambo. Elimu ndiyo msingi wa maisha (Kipyegon, 2017). Ufanisi wa elimu kwa mtoto huchangiwa na aina ya malezi anayoyapata kutoka kwa walezi wake. Hali hii inatokana na kwamba mzazi ni mwali muwa mwanzo wa mtoto. Katika kumlea mtoto kuna mahusiano na namna mtoto huyo anavyolelewa. Hivyo, humuathiri katika namna hasi ama chanya katika kujifunza kwao.

Watoto wa kiume wa jamii ya Wazanzibari kupitia riwaya teule wanaonekana kama kundi moja wapo linalokosa haki yake ya msingi ya elimu. Kitendo cha mtoto huyu kukosa haki yake hiyo ndiko kulikochangia kuchupa mipaka. Msanii Adam Shafi ameonesha jinsi malezi yanavyoathiri ujifunzaji wa watoto wao.

Kupitia riwaya ya *Mtoto wa Mama* mwandishi anatuonesha Saburi na Shauri wakiwa mionganoni mwa watoto wa kiume wa jamii ya Wazanzibari waliokosa elimu. Mathalani, mwandishi amemtumilia Saburi pale alipolikuta kundi la watoto wa skuli waliotumia muda wao wa mapumziko kucheza michezo yao. Alijiunga pamoja nao kwa ajili ya kucheza michezo mbalimbali lakini baada ya muda Saburi alijikuta akiwa pweke baada ya kengele iliyowataka watoto wale wakamalizie vipindi vyao vya masomo vilivyobakia. Walimwacha Saburi akiwa peke yake. Kama mtoto hali hii ilimtia simanzi Saburi. Kuhusu hili mwandishi anasema:

...Ule ulikuwa ni muda wa mapumziko kwa watoto wa skuli na mlio ule wa kengele uliwapa ishara kuwa muda wa mapumziko ulikuwa umekwisha na ukiwaita wakaendelee na masomo. Kwa hivyo wote walikimbilia skuli. Saburi alihisi kama kwamba watoto wale wote walikimbilia yeye na kwamba yeye hastahiki kucheza nao. Hilo lilimtia unyonge mkubwa (uk. 55 - 56).

Dondoo hili linaonesha namna Saburi alivyohuzunika kwa kukimbiwa na kundi la watoto kama yeye. Watoto hao walielekea shule kumaliza vipindi vyao vya masomo ya siku kwa muda uliobakia na kumwacha Saburi hali ya kuwa ameduwaa. Kukosekana kwa elimu kwa mtoto Saburi kulimsababisha mtoto huyo kushirikiana na kundi ovu la wahuni na walevi wa Mbele ya Njia Kuu. Katika hali hiyo Saburi anajikuta ameduwaa hajui la kufanya pale watoto wa shule walipomwacha peke yake.

Watoto Wenyenyewe Wanakuwa Wakaidi

Baadhi ya watoto maumbile yao ni wakaidi na tayari nafsi zao zimekwishaharibika. Wanapoelekezwa au kukatazwa jambo fulani na wazazi wao lililo baya huwa wanakataa maelekezo hayo. Huendelea na tabia yao hiyo ya uasi na matokeo yake yanakuwa hayardhishi. Licha ya wazazi wao kuchukua jitihada za makusudi kuwaelekeza waongoke na wafuate mwelekeo uliosawiya, ndivyo hivyo hivyo watoto hao wanapozidi ari ya kuendeleza uasi huo bila kufikiria mwisho wake litatokea nini au watakutwa na lipi.

Hii inatokana na nafsi za watoto hawa kuharibika. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* tunaona kwamba licha ya Zamda kujitahidi katika malezi ya mtoto wake, ndivyo mtoto huyo alivyokithiri kurudia tena kosa hilo ambalo alitakiwa aliache. Hali hiyo imejitokeza katika uk. 38, 39, 40, 50, 75, 77, 78, 79, 83, na 85. Zamda, mama mzazi wa Saburi hakuacha kumwelekeza Saburi mienendo inayofaa hadi alipobaini kuwa Saburi amemshinda na hamwezi tena. Kuanzia hapo alimwachia tu afanye apendavyo na huku akisubiri majaliwa yake. Maelezo ya mwandishi ni ithibati tosha kuhusu ukaidi wa mtoto huyo.

Kadri Saburi anavyokatazwa na mama yake juu ya tabia yake ya kutoka na kutokomea mbali ya macho ya mama yake ndivyo alivyopanda mori. Zamda baadhi ya wakati aliquwa mkali sana kuhusu suala hili. Saburi hakupenda kusema alipokuwa, jambo hilo lilimzidisha hasira mama yake. Zamda anamwuliza mtoto wake:

“Ulikuwa wapi tokea asubuhi?” Alimwuliza. Saburi alinyamaza kimnya huku akimtzama mama yake kwa macho yake madogo yaliyojaa utoto huku akitafuna kucha za vidole vyake vya mkono.

“Leo umegeuka bubu? Hujui kusema. Nakualiza ulikuwa wapi tokea asubuhi?” Zamda alimwuliza tena mara hii kwa ukali. “Sikuwa mahali mama”, alijibu Saburi. “Hukuwa mahali? Hukuwa mahali n’do

manake nini?" Aliuliza Zamda kwa ukali zaidi, macho ameyatumbua anamtazama Saburi." Nakuuliza ulikuwa wapi tokea asubuhi. Nataka kupajua hapo ulipokwenda, ukazama jii, kutwa, mpaka saa hizi. " Saburi aliendelea kunyamaza. Kama hutaki kusema ngoja. Utanitambua mwana kuni za mkandaa we... " "Utasema leo huko ulikokuwa kutwa nzima!" Saburi alipiga kelele akilia huku akisema," Basi mamaaa! Nitasema! Nitasema!" .Sema ulikuwa wapi?" Zamda aliendelea kupiga kelele huku akimchapa Saburi zaidi (uk. 40).

Tukilichunguza dondoo hilo, tunapata kujua kuwa mzazi wa kike hutumia juhudi, nguvu, ukali, vitisho na vipigo kama ni baadhi ya njia za kumfundisha mtoto wake huyo mipaka ya kucheza kwake na kuchangamana na watoto wenzake. Njia hiyo ya kimalezi katika wakati huu tulionao inaonekana kuwa haifanyi kazi ipasavyo. Tunamuona Zamda baadhi ya wakati akimkataza mtoto wake, na wakati mwingine anamlea mtoto huyo kwa namna tofauti.

Zamda baada ya kugonga mwamba anamuuliza Saburi amueleze kwa dhati yake amweleze amfanyeje kutokana na kuwa tayari ameshamaliza mbinu zake za malezi lakini hajafanikiwa. Mwandishi anaeleza:

Alipomwona Saburi tu, alimchupia kwa maneno, Mtoto weye!" Alimpigia kelele. Sijui nikufanye nini. Juzi tu nilikupiga kwa hulka yako hiyohiyo ya kutoka ukapotea jii! Leo tena umerudia yaleyale," alimwambia, wewe Saburi kwani ni husikii?" Hapo tena ikawa zamu ya mzee Hamisi kumkaripia Saburi. Wewe endelea tu, siku nitakayokuja kukutia mimi mkononi, utashika adabu yako." (uk. 49 - 50).

Dondoo hilo linathibitisha kuwa licha ya wazazi na walezi kujifunga mkaja na kupania kuwaelekeza watoto wao katika maadili mazuri bado kuna changamoto kubwa kwa walezi na wazazi kwa watoto. Hata hivyo, utafiti umeonesha kuwa malezi kwa watoto wa kiume yamekabiliwa na changamoto nyingi zinazosababishwa na wigo mpana ukiwemo mazingira, makundi na wakati mwingine watoto wenyewe kama ilivyodhahirika hapo juu.

Wakati wazazi wanawapa mwongozo wa maisha na kuwachunga watoto wao wa kiume kuepukana na tabia mbaya, mazingira ya mitaani yanaruhusu watoto hao kutoka nje ya mitaa yao na kutafuta watoto wingine kucheza nao pamoja au kufanya kazi nyingine. Kitendo cha watoto wa kiume kuwa mbali kimasafa wakiepukana na wazazi wao huweza kuwachochea kufanya mambo yasiotarajiwa na jamii. Pia, imegundulika kuwa wazazi wanaotumia vitisho, nguvu na ukali huwafanya watoto wao kuwa sugu na mwishowe kutokuogopa.

Aidha, kuna maandiko mbalimbali yanayoelezea elimu ya malezi na makuzi ya mtoto, changamoto zao na mbinu za kukabiliana nazo, zikiwemo changamoto za kimazingira wanazokumbana nazo watoto wa kiume. Changamoto hizo ni pamoja na makundi maovu, matumizi ya madawa ya kulevya, ulawiti, wizi na ujambazi.

Pia, simu za mkononi na mitandao ya kijamii, yamebeba dhima ya malezi ya watoto. Matumizi mabaya ya makundi na mitandao ya kijamii huweza kuwasababishia watoto wa kiume waende ndivyosivyo kutokana na kupotoka kimaadili, hii inatokana na ujumbe wanaopokea watoto hao. Baadhi ya ujumbe unaopatikana kuititia mitandao ya kijamii na ushawishi wa makundi rika hauendani na mila, silka na desturi za jamii ya Wazanzibari. Picha za uchi hurushwa katika mitandao na watoto wa kiume katika makundi yao huzipakuwa na baadae kuzisoma na kuziangalia na mwishowe hufanyiwa mazoezi. Ni katika muktadha huo, wazazi hukumbana na changamoto kubwa katika kuwalea watoto wao wa kiume.

Migogoro kati ya wazazi au walezi na watoto wao inajitokeza kila uchao kutokana na tofauti ya tamaduni za Wazanzibari na zile tamaduni za kigeni. Hivyo basi, hali hiyo itakapofumbiwa macho na kutokuangaliwa kwa umakini wake watoto wa kiume watakwenda ndivyo sivyo na inawezekana kupotoka kabisa.

Hitimisho

Makala haya yanahitimisha kwa kusisitiza kuwa malezi ya watoto hasa wa kiume bado ni changamoto katika jamii. Ili mambo yaende vizuri kunahitajika ushirikiano wa hali ya juu katika kuwafanya watoto hao wafikie matarajio ya wazazi wao na jamii kwa ujumla. Kufanya hivyo ndiko kutakakoyafanya malezi ya watoto hao kuwa sawia. Kama ilivyokwisheshaelezwa hapo awali kuwa adui mkubwa anayevuruga mchakato mzima wa malezi ya watoto hao ni kuwepo kwa suala zima la mwingiliano wa tamaduni na sayansi na teknolojia katika wakati huu tulonao, akini jamii bado haijamka ikapata uelewa wa kutosha kutokana na janga hili. Makala yameweza kufafanua jambo hili kuititia riwaya teule na kujadili sababu mbalimbali zinazosababisha upogo wa malezi ya mtoto huyo wa kiume. Ili kupunguza tatizo hili la upogo wa malezi ya mtoto wa kiume, wazazi na walezi, watoto na jamii kwa pamoja hawana budi kushirikiana na kuchukuwa jitihda mbalimbali ili kulinusuru taifa hilo change kama wanavyozungumza wahenga kwamba, watoto ndio taifa la kesho.

Marejeleo

- BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- Bayyo, F. (2020) *Usawiri wa Jinsi ya Kiume katika Riwaya Teule za Shafi Adam Shafi*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Comte, A. (1839) *Founder of sociology*. New York: Routledge.
- Frances, J. (2018) “Parenting Style in Relation to Social Economic Status, Education and Generation”. Inapatikana katika <https://www.nation.co.ke/lifestyle/saturday/flakes-parenting-the-kenyan-way>. Ilisomwa tarehe 28/2/2023.
- Gitau, E. N. (2005) *Unyanyasaji Dhidi ya Wanaume katika Fasihi Andishi ya Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Kenya: Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Jilali, H. (2010/2011). “Lugha na Jinsia katika Ushairi: Uchunguzi wa Sitiari za UKIMWI na Mapenzi katika Mashairi ya Bongo Flever”. *Mulika*, Juz. 29&30 (1): 54-68.
- Kavuria, P. (2008) *Dhuluma Dhidi ya Watoto katika Riwaya za Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Kenya: Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Khatibu, M. (2014) *Chanjo, Matakwaa ya Mwanamume katika Mwili wa Mwanamke*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Kipyegon, H. (2017) “Influence of Parenting to Child Education.” Inapatikana katika <https://www.kenyaplex.com/resources>. Ilisomwaa tarehe 29/6/2023.
- Kobia na Mung’ahu, R. (2013) “Ubabedume katika Ushairi wa Kiswahili: Mfano wa Utensi wa Fumo Liyongo”. *Kioo cha Lugha*, Juz. 11 (1): 14-29.
- Kobia, J. (2008) *Taswira za Kiuana katika Nyimbo za Tohara za Wanaume Mionganini mwa Waigembe*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Kenya: Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Mbogo, E. (2005) *Watoto wa Mama N’tilie*. Dar-es-Salaam: HEKO Publishers Ltd.
- Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Nairobi: Sitima Printer and Stations L. t.d.
- Mosha, D. F. (2018) “Athari za Mgawanyo Tofauti wa Majukumu ya Kijinsia katika Nyimbo za Watoto kwa Watoto”. *Mulika*, Juz. 37 (1): 87-105.
- Ngwiri, L. (2008) *Powerful Parenting: What Every Parent Should Know*. Nairobi: Queennex Holding Ltd.
- Noordin, M. N. (2017) *Lugha na Ujinsia katika Jamii katika Lugha na Fasihi katika Karne ya Ishirini na Moja*. Nairobi: Moi University Press.
- Omari, S. (2008) “Fasihi simulizi na jinsia: Mifano kutoka nyimbo za watoto Tanzania”. *Kioo Cha Lugha*, Juz. 71(1): 77-102.
- Othman, Z. O. (2018) *Kuchunguza Fani na Dhamira ya Malezi ya watoto katika Riwaya ya Kiswahili: Mfano Riwaya ya Watoto wa Mama N’tilie*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Santrock, J. (2007) *A Topical Approach to life Span Development*. New York: Mc Graw-Hill.
- Shafi, A. (2008) *Kasri ya Mwinyi Fuad*. Nairobi: Vide~ Muwa Publishers Limited.
- Shafi, A. (2013) *Mbali na Nyumbani*. Nairobi: Sasa sema.
- Shafi, A. (2018) *Mtoto wa Mama*. Rwanda: Longhorn Publishers.